# UMOJA - JARIDA

UNITED NATIONS
TANZANIA

Toleo No. 92
Septemba - Octoba 2020


## ZANZIBAR YAZINDUA MKAKATI WAKE WA AFYA DIJITALI



Mkakati mpya wa afya dijitali wa Zanzibar utawezesha usambazaji habari/taarifa kuhusu huduma za afya za kila siku na za dharura ili kuimarisha ubora wa matunzo ya afya visiwani humo. ***Picha | WHO Tanzania***

## VIDOKEZO


- Republic of Korea, UNFPA and UN Women partner to advance gender equality for some of the furthest behind women and girls in Tanzania
- Local Women contribute to combating COVID-19 in their Community
- UN capacitates CHVs on COVID-19 knowledge
- Innovative 'keyhole' gardens help refugees improve their nutrition


Katika jitihada za kuongeza upatikanaji wa huduma bora za afya, Wizara ya Afya ya Zanzibar hivi karibuni imezindua mpango mkakati wake wa afya dijitali. Mpango mkakati huo wa miaka mitano (2021 - 2025) ulizinduliwa na Waziri wa Afya, Mh. Hamad Rashid, huko Unguja.

Mpango huo unaoana vema na Lengo la Tatu la Malengo ya Maendeleo Endelevu la kuhakikisha afya bora na kushajiisha ustawi wa maisha ya watu wote wa marika yote. Mkakati huo utaongoza matumizi ya teknolojia za kidigitali za afya zinazowezesha utoaji wa huduma za afya zilizo salama, zenye usawa, zinazopatikana kwa wote, zenye ufanisi na zenye kufaa katika ngazi zote.

Mkakati wa Afya Dijitali unaoana na Mkakati wa Pili wa Kukuza na Kupunguza Umaskini Zanzibar (MKUZA II) na unakamilisha masuluhisho ya afya ya kidijitali yanayoendelea kutekelezwa, yaani, Mfumo wa Taarifa za Afya wa Wilaya (DHIS2), Mfumo wa Kielektroniki wa Kuendesha Lojistiki za Taarifa (eLMIS) na Mfumo wa Kufuatilia Malaria. "Mkakati unatoa mwelekeo wa mageuzi katika mfumo mzima wa afya kwa lengo la kuongeza matumizi ya mifumo ya ngazi za wateja yanayowezesha utoaji wa huduma salama na bora za afya," alisema Mkurugenzi Mkuu, Wizara ya afya, Dkt. Jamala Taib.

Hatua hii kubwa inaiunganisha Zanzibar na zaidi ya nchi na madola mengine 120 kote duniani yaliyoandaa sera na mikakati kuhusu huduma za kielektroniki za afya (eHealth).

***Inaendelea Ukurasa wa 2***

This newsletter is published by the UN Communication Group in Tanzania. To subscribe and provide feedback, please contact us at: info.untz@one.un.org | Website: tanzania.un.org | Tel: (+255) 22-219-5021

*Kutoka ukurasa wa 1*

Shirika la Afya Duniani (WHO) pamoja na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Denmark (DANIDA), USAID, PATH na D-Tree International yalifadhili uanzishwaji na uzinduzi wa makakati huo.

Ofisa Mwakilishi wa WHO huko Zanzibar, Dkt. Ghirmay Andemichael, aliipongeza Zanzibar kwa kuanzisha na kuzindua mpango mkakati wa afya wa kidijitali. Alisema mpango huo ulidhihirisha utayari wa Zanzibar kuimarisha upatikanaji na ubora wa huduma za afya.

Afya dijitali ni matumizi ya teknolojia za habari na mawasiliano (TEHAMA) na mtu mmoja mmoja, watoa huduma za afya, mifumo ya afya ili kuongeza upatikanaji, ueneaji, ubora, na unafuu wa gharama wa taarifa za afya na utoaji huduma kwa wote. Azimio la mwaka 2005 la Baraza Kuu la Afya duniani lilizitaka nchi wanachama kuzingatia uanzishwaji wa mipango mikakati ya muda mrefu ya kuunda na kutekeleza huduma za Afya Elektroniki ili kushajiisha manufaa yenye haki, ya gharama nafuu na yanayo patikana kwa wote.

Kwa kuongezea, Baraza Kuu la Afya Duniani, mwaka 2013 lilipitisha Azimio la viwango na mwingiliano wa Huduma Elektroniki. Azimio la kufuatia hilo lilizitaka nchi wanachama kuanzisha sera na mbinu za kisheria ili kuongoza afya dijitali katika nchi zao.

## KUPITISHA MBINU YA SEKTA NYINGI KATIKA KUPAMBANA NA KIPINDUPINDU

Mapema mwezi Septemba, Wizara ya Afya upande wa Tanzania Bara ilianzisha juhudi za kukamilisha maandalizi ya Mpango wa Taifa wa Sekta Nyingi wa Kuzuia na Kudhibiti Kipindupindu (NMCPCP).

Umoja wa Mataifa kupitia ofisi ya nchi ya Shirika la Afya Duniani (WHO) ilifadhili maandalizi ya mpango huo. Ushiriki wa wadau mbalimbali katika mipango na utekelezaji wa programu ya afya ni muhimu ili kuleta maendeleo kuelekea utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) ya Umoja wa Mataifa yanayohusiana na afya.

Kupitisha matumizi ya mbinu ya sekta nyingi ili kupambana na kipindupindu, mpango huo unabaini na kuimarisha ushirikiano miongoni mwa idara za serikali, washirika wa pande nyingi na wa pande mbili na asasi zisizo za kiserikali (AZAKI), ambazo juhudi zao zote zinachangia kupunguza na kuzuia maambukizi ya kipindupindu katika ngazi za mtaa/kijiji na kitaifa.

Mchakato wa kuandaa mpango huu ulianza mwaka 2019 ukihusisha warsha za mashauriano kati ya wadau mbalimbali na kufikia kilele katika warsha iliyoandaliwa hivi karibuni huko Arusha ili kuhitimisha mpango huo. Kupitia mbinu ya ushirikishaji sekta mbalimbali pamoja na uratibu mzuri wa majukumu na kazi za washirika tofauti, mpango pia unalenga kupunguza uuguaji sugu na vifo vinavyotokana na kipindupindu kwa asilimia 90, na kudhibiti na kuzuia maambukizo ya kipindupindu.

Kitengo cha Kuratibu Udhibiti wa Majanga katika Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa walihusishwa katika machakato wa kuandaa mpango mkakati huo, kwa hiyo kuupa mpango huo mpya jukwaa la kuwa na uratibu na ushiriki wenye tija zaidi wa wizara na idara za sekta zote zinazohusika katika ngazi za Serikali Kuu na Mamlaka za Mitaa.

Mpango huu wa sekta nyingi umeandaliwa kwa kutumia taarifa ya Mapitio ya Baada

*Inaendelea Ukurasa wa 3*

*Kutoka ukurasa wa 2*

ya Tukio (AAR) yaliyofanyika mwezi Agosti, 2017 na mafunzo yatokanayo wakati wa mwitiko wa awali dhidi ya mlipuko wa kipindupindu. Mpango huu unalenga kupambana na kipindupindu nchini Tanzania kupitia mbinu zinazoratibiwa vizuri za sekta mtambuka na zinazosisitiza juhudi za kuendelea kuzuia kulinganisha na mkazo wa kimazoea wa mwitiko tu dhidi ya kipindupindu. Juhudi hizi zinalenga katika maeneo 17 yaliyo hatari zaidi kwa kipindupindu yanayohusiana na yale yanayoathiriwa na mafuriko na ukame mara kwa mara, maeneo ya makazi ya wenye kipato duni mijini, kambi za wakimbizi, na juhudi za kuvuka mipaka.

Mpango unakazia zaidi pia katika vipaumbele vya juhudi zinazotokana na ushahidi wa utafiti zikiwemo: uratibu wa sekta mchanganyiko, ufuatiliaji na maabara, maji, usafi na mazingira (WASH) na uhamasihaji jamii na ushiriki wa jamii. Ili kuondokana na utegemezi katika mfumo mkuu wa uendeshaji, mpango unasisitiza uimarishaji wa uwezo katika ngazi za chini wa kubaini, kusimamia, kudhibiti na kuzuia kipindupindu.

"Mpango uliofanyiwa mapitio unatatua changamoto za mipango iliyopita kwa kuzingatia ushahidi uliotokana na utafiti na mapendekezo kutoka katika sekta mbalimbali na kutoka katika mpango wa dunia wa kukomesha kipindupindu ifikapo mwaka 2030," alisema Dkt. Leonard Subi, Mkurugenzi wa Huduma za Kinga katika Wizara ya Afya.

Mpango wa miaka mitano (2019 -2023) unalenga kuweka msingi na mkakati wa kumaliza kipindupindu nchini Tanzania na hivyo kufikia lengo la dunia la kukomesha kipindupindu ifikapo mwaka 2030. Kipindupindu kinazidi kuwa tatizo kubwa la kiafya nchini Tanzania. Muda mrefu zaidi wa ugonjwa huo kudumu ilikuwa kutoka Agosti 2015 hadi Desemba 2018, na ugonjwa uliathiri mikoa 26 na wilaya 129 (kati ya 139) nchini Tanzania.



Ofisa Mfuatiliaji wa WHO akitoa mafunzo kwa mtumishi wa afya ya jamii kuhusu ufuatiliaji magonjwa katika jamii. WHO ilishirikiana na Wizara ya Afya ya Zanzibar kugatua uendeshaji wa Kituo cha Shughuli za Dharura za Afya ya Jamii. ***Picha | WHO Tanzania***

# JAMHURI YA KOREA, UNFPA NA UN WOMEN KUSHIRIKIANA KUENDELEZA USAWA WA JINSIA KWA BAADHI YA WANAWAKE NA WASICHANA WALIO NYUMA SANA NCHINI TANZANIA




Mashirika dada ya Umoja wa Mataifa -- UNFPA na UN Women – yanatumia rasilimali zao kuendeleza usawa wa jinsia katika mikoa ya Singida na Shinyanga. ***Picha | UNFPA Tanzania/UN Women Tanzania***

Mwishoni mwa mwezi wa Septemba, mashirika ya UNFPA na UN Women yalizindua Programu ya Pamoja yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 5 utakaodumu kwa miaka mitatu “Kuleta Usawa wa Kijinisia kupitia Uwezeshaji Wanawake na Wasichana walio katika umri wa balehe” katika Wilaya ya Msasala, Mkoa wa Shinyanga, Tanzania, kwa msaada wa Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Korea (KOICA). Programu hii inafuatia nyingine kama hiyo iliyozinduliwa huko Wilaya ya Ikungi, Mkoa wa Singida tarehe 29 Septemba.

Uzinduzi wa Programu Hii ya Pamoja ni matunda ya mchakato wa mashauriano ya miaka miwili kwa kushirikisha washirika wa kitaifa na wa hapa nchini, ambapo utatumia nguvu ya ushawishi ya mashirika dada yaani UNFPA na UN Women kuendeleza juhudi za usawa wa kijinsia katika wilaya za Ikungi na Msasala na kwa upana zaidi katika mikoa ya Singida na Shinyanga ili kuhakikisha kwamba wanawake na wasichana wa vijijini hawaachwi nyuma.

Licha ya hatua zilizokwishapigwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kukabili ukosefu wa usawa na ubaguzi wa kijinsia, kama inavyoelezwa bayana katika ajenda za maendeleo za kitaifa, kikanda na dunia, ukatili wa kijinsia, kisaikolojia, kimwili na kiuchumi vinabaki kuwa uhalisia wa kila siku katika maisha ya wanawake na wasichana wengi katika mikoa ya Singida na Shinyanga.

Ubaguzi na ukosefu wa usawa wa kijinsia vilivyokubuhu vikiendelezwa na kaida zenye mizizi mirefu vinaendalea kuchochea ukatili, ukiwemo ukeketaji na ndoa za mapema, na za lazima za utotoni, ambapo wanawake na wasichana wanaendelea kubeba mzigo mzito mno wa kazi za nyumbani.

***Inaendelea Ukurasa wa 5***

*Kutoka ukurasa wa 4*

Matokeo ya umaskini wa muda, ukosefu wa elimu, na ukosefu wa umiliki mali na ufikiaji wa huduma za kifedha kwa pamoja yanawakosesha fursa na ushiriki wa wanawake na wasichana katika maisha ya jamii na kazi zenye tija.

Juhudi zitakazotokana na programu hii zitalenga kutatua kaida za kijamii zinazoendelea kuwafunga wanawake na wasichana katika mduara wa ukosefu wa haki na ukatili na badala yake kuwawezesha kushiriki katika maisha ya kiuchumi na kijamii kikamilifu.

Kujenga mazingira wezeshi zaidi kwa wanawake kumiliki ardhi na kwa wakulima wadogowadogo wakiwemo wanawake vijana kushiriki na kuwa na tija zaidi katika sekta ya kilimo yatakuwa miongoni mwa malengo, kama itakavyokuwa kwa uimairishaji mifumo ya kuzuia na kutoa mwitiko dhidi ya ukatili wa kijinsia na kuweka mifumo ya kijamii na mazingira salama yatakayoongeza ushiriki chanya wa wanawake an wasichana na uwezo wa kuendeleza haki zao.

Programu hii ya Pamoja ni sehemu ya Mpango wa Pili wa Msaada wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa (UNDAP II), ambao unaisaidia Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufikia malengo yake katika dira yake ya taifa na unaendana na miundodhana ya mikakati ya kitaifa kuendeleza usawa wa jinsia na uwezeshaji wanawake.

Usawa wa jinsia na uwezeshaji wanawake na wasichana ni vipaumbele vya ushirikiano wa maendeleo wa Korea. Shirika la Ushirikiano wa Maendeleo la Korea limefanya kazi kwa karibu na washirika mbalimbali, yakiwemo mashirika ya Umoja wa Mataifa, nchini Tanzania na kushughulikia baadhi ya changamoto nzito ambazo wanawake na wasichana wanakabiliana nazo katika afya na elimu.

## KUONGOZA KWA MFANO! UNICEF TANZANIA YATUMIA UMEME JUA KATIKA JUHUDI ZA KUELEKEA KATIKA MATUMIZI RAFIKI YA NISHATI KUPUNGUZA HEWA UKAA



Mtambo wa umeme jua ulifungwa kwa mafanikio katikati ya mwaka 2019 katika majengo ya ofisi za UNICEF Tanzania, jijini Dar es Salaam, kwa lengo la kupunguza uzalishaji wa hewa ya ukaa ili kuwalinda wale walio hatarini zaidi kati yetu – watoto wetu. ***Picha | UNICEF Tanzania***

Mwaka huu ulianza vizuri kwa UNICEF Tanzania ambapo ofisi hiyo ilichukua hatua chanya kupunguza uzalishaji wake wa hewa ya ukaa. Tafiti zimeonyesha kwamba uzalishaji hewa ya ukaa kutoka katika majengo na miundombinu ya namna hiyo ndiyo chanzo kikuu cha Umoja wa Mataifa cha utoaji hewa ukaa baada ya vyombo vya usafiri.

Ili kupunguza athari zake katika mazingira, UNICEF Tanzania imeanzisha mpango

*Inaendelea Ukurasa wa 6*

*Kutoka ukurasa wa 5*

kazi wa miaka miwili wa ufanisi na ufikikaji katika mazingira rahisi. Mpango kazi huo unajumuisha utekelezaji wa hatua za uimarishaji matumizi yenye ufanisi ya nishati katika majengo yaliyojengwa na kumilikiwa na UNICEF jijini Dar es Salaam. Jambo hili litakuwa na mchango mkubwa katika kupunguza uzalishaji wa shirika wa hewa ukaa na kufikia mwoanisho unaofaa kwa tabia ya nchi.

Aliyekuwa Naibu Mwakilishi (Uendeshaji) wa UNICEF Tanzania, James Gitau, alisema, “Tuliamua kuyatumia majengo mapya ya ofisi kuimarisha matumizi rafiki ya nishati jambo lililozaa utafiti wa mwanzo wa kupima uwezekano ili kuamua juu ya ufumbuzi bora wa nishati jua na hatimaye ufungaji wa paneli za umeme jua. Uamuzi huu wa kuhamia kwenye nishati mbadala unaimarisha ahadi yetu kama UNICEF kupunguza athari yetu hasi katika mazingira ikiwemo uzalishaji wa hewa ukaa kutokana na shughuli zetu za uendeshaji.”

Baada ya utafiti wa awali kuona uwezekano mwaka 2018, iliamriwa kufunga mifumo ya nishati jua ya 105KW katika paa la majengo ya ofisi. Mahali iliko Tanzania kijiografia inaifanya nchi kuwa pahali bora kunufaika na ufungaji wa mitambo ya umeme jua. Mtambo



Mradi wa umeme jua unachangia kufikia malengo ya kidunia ya UNICEF ya kupunguza uzalishaji wake wa hewa ukaa ambapo kupitia mradi huo UNICEF itaokoa tani 170 - 210 za hewa ukaa kila mwaka, hivyo kuchangia katika kuweka mazingira safi kwa ajili ya hatma ya watoto wetu. ***Picha | UNICEF Tanzania***

huo unaiwezesha ofisi ya UNICEF Tanzania kutimiza mahitaji yake yote ya nishati na hutumia tu umeme wa gridi ya Taifa katika siku za mawingu na usiku.

Naibu Mwakilishi (Programu) wa UNICEF Tanzania, Rene Van Dongen, alisema, “Huu ulikuwa mpango wenye shauku kubwa kwetu, na timu nzima ilifanya kila jitihada ili kufanikisha uhamiaji huu katika vyanzo vya nishati mbadala. Hii ni hatua kubwa kwa UNICEF Tanzania kwani mtambo huu wa umeme jua utapunguza uzalishaji wa hewa ukaa kwa takribani kilo 170,000-210,000 kwa mwaka, jambo litakalomaanisha uwekezaji mkubwa wenye athari chanya kwenye mazingira.”

Mwakilishi wa UNICEF Tanzania, Shalini Bahuguna, aliipongeza timu nzima kwa mafanikio haya. Alisema, “Sote tunapaswa kutimiza wajibu wetu katika kujenga mazingira yanayofaa kwa watoto. Mabadiliko ya tabia ya nchi yanatuathiri sisi sote na wengine wanaathirika hata zaidi. Hii ni juhudi ndogo lakini njema katika kuimarisha matumizi ya nishati rafiki kwa mazingira na inachangia katika lengo la kidunia la UNICEF la kupunguza uzalishaji wetu wa hewa ya ukaa. Huu ni wajibu wetu wa msingi kwa watoto wetu na vizazi vijavyo.”

# UBUNIFU WA BUSTANI ZA MSINGI UNAVYOIMARISHA LISHE YA WAKIMBIZI



Vanencia akivuna mbogamboga kutoka katika bustani yake ya msingi katika Kambi ya Wakimbizi ya Nduta iliyoko Mkoa wa Kigoma. ***Picha* | ©*DRC/Christina John***

Venancia Nibitanga anakuja kutokea nyuma ya nyumba yake akiwa amebeba fungu la mboga za majani. Anaanza kuziosha na kuzikatakata tayari kwa mapishi. Binti yake mdogo anafuatilia kwa makini kila hatua. "Nafikiri atakuja kuwa mpishi hodari, kama alivyo mama yake," anasema Venancia.

Venancia alikimbia Burundi mwezi Aprili, 2016, baada ya mumewe kuwa mkatili kupita kiasi kwake na kwa watoto wake. "Baada ya mgogoro wa kisiasa wa mwaka 2015, baba huyo aliongeza ukatili. Watoto wangu na mimi tuliondoka Burundi bila chochote ukiacha nguo tulizokuwa tumevaa," anasimulia.

Hivi sasa ana furaha kwamba yeye ni miongoni mwa familia 1,300 ambazo zimehusishwa katika mradi wa uzalishaji mbogamboga. Mradi huo unajulikana kama bustani ya msingi, ambayo ni bedi la duara lililotengenezwa kwa vifaa vya gharama nafuu na vinavyopatikana kirahisi. Kupitia mradi huu, Shirika la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR) na Baraza la Wakimbizi la Denmark (Danish Refugee Council) kwa pamoja yanazisaidia familia za wakimbizi kuanzisha bustani hizi, na kuwapa mbegu, vifaa na mafunzo kuhusu mipango bora ya kilimo-tija.

Kabla ya mradi huo, Venancia mwenye miaka 35, alitegemea tu migao ya chakula iliyotolewa pale kambini, ambapo kiwango chake sasa kimepungua hadi kufika asilimia 72 ya mgao wa chakula ili kulisha watoto wake saba. "Tunashukuru kwa chakula tunachopata, lakini kilikuwa hakitoshi na hakikuwa na mbogamboga," anasema.

> *"Tulikula mlo mmoja kwa siku kwa sababu niliogopa kuwa mgao wetu wa mwezi ungaliisha mapema kabla ya muda, sasa familia ina chakula cha kutosha, na kina virutubisho zaidi,"*
>
> **Venancia Nibitanga, Mkimbizi kutoka Burundi, Tanzania**

***Inaendelea Ukurasa wa 8***

*Kutoka ukurasa wa 7*

“Tulikula mlo mmoja kwa siku kwa sababu niliogopa kuwa mgao wetu wa mwezi ungaliisha mapema kabla ya muda, sasa familia ina chakula cha kutosha, na kina virutubisho zaidi,” anasema huku akitabasamu.



Venancia na familia yake wakifurahia mlo wa mbogamboga kutoka katika bustani yake ya msingi katika Kambi ya Wakimbizi ya Nduta, Mkoa wa Kigoma. ***Picha* | *©DRC/Christina John***

Kupungua kwa mgao kunatokana na marekebisho ya gharma ili kuendana na ongezeko la gharama za usambazaji kulitokana na mahitaji ya kukabili hatari za maambukizo ya COVID-19. Jumla ya Dola za Marekani milioni 21 zinahitajika ili kuhakikisha kwamba wakimbizi watapata mgao wao kamili wa chakula kwa mwezi kati ya sasa na mwezi Machi, 2021.

Huku fursa zikizidi kuwa haba za kujipatika kipato cha kujikimu, wakimbizi nchini Tanzania karibu wanategemea misaada ya kiutu kwa kila kitu. Miradi kama hiyo ni muhimu na inahakikisha kwamba wakimbizi 240,000 wanaoishi Tanzania wanakuwa na mchango chanya katika kuhakikisha usalama wao wa chakula na lishe.

“Chakula na malazi ndiyo mahitaji ya msingi kabisa ya kibinadamu. Ile hadhi ya utu, hata hivyo, inakuwa haipewi nafasi yake kwa kuwafanya makundi ya watu kuwa wategemezi wa misaada ya chakula ambacho daima nacho hakitoshelezi, na ambacho kiutamaduni hakikuzoeleka,” anasema Antonio Canhandula, Mwakilishi wa UNHCR nchini Tanzania.

## UN YAJENGA UWEZO WA MAOFISA AFYA WA KUJITOLEA KUHUSU MAARIFA YA COVID-19

Baada ya mgonjwa wa kwanza wa COVID-19 kuthibitishwa Zanzibar, juhudi kubwa zilianzishwa ili kukabiliana na kuenea kwa ugonjwa huo. Miongoni mwa mikakati muhimu katika kubadilishana taarifa ulikuwa kuendeleza mbinu zilizopo za usambaji taarifa katika ngazi ya jamii, ambayo ilihusisha matumizi ya watumishi afya wa kujitolea (CHV).

Katika suala hili, UN iliendelea kuwasaidia watumishi hawa ili wazisaidie jamii kuelewa mbinu za kujikinga dhidi ya COVID-19. Kwa namna ya pekee, UNICEF kwa kushirikiana na shirika la Save the Children yaliisaidia Wizara ya Afya kujenga uwezo wa watumishi afya wa kujitolea wapatao 1,300, na wasimamizi wao 80 kuhusu utoaji wa ujumbe wa kuzuia COVID-19 na kuhusu mwendelezo wa huduma za msingi katika muktadha wa COVID-19.

Ili kuwalinda wafanyakazi hawa waliokuwa mstari wa mbele, UNICEF ilinunua vifaa vya kujikinga na maambukizo (barakoa, vitakasa mikono na viatu vya kufunika)

*Inaendelea Ukurasa wa 9*

*Kutoka ukurasa wa 8*

vyenye thamani ya Shilingi milioni 260 kwa ajili ya watumishi afya wa kujitolea na watoa huduma za afya waliokuwa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja na kwa ajili ya matumizi katika vituo vya kutenga wagonjwa ili kuzuia kuenea kwa COVID-19. Licha ya hayo, watumishi afya wa kujitolea 680 kutoka Unguja na Pemba walipata mafunzo chini ya Shirika la Afya Duniani (WHO) kuhusu ufuatiliaji wagonjwa katika jamii.

Kama chanzo cha maarifa, watumishi afya wa kujitolea waliwashirikisha wengine machapisho ya elimu; walisadia ufuatiliaji wagonjwa katika jamii; na walitoa nasaha kwa walioathirika na COVID-19. Umoja wa Mataifa unaendelea kuwasaidia watumishi afya wa kujitolea ili wazisaidie jamii kuelewa namna ya kujikinga dhidi ya COVID-19.





Kipindi cha mafunzo kwa watumishi afya wa kujitolea huko Zanzibar kikiendelea ili kusaidia juhudi za kuzuia kuenea kwa COVID-19. ***Picha | UN Tanzania***

## WANAWAKE WENYEJI WACHANGIA KATIKA KUKABILI COVID-19 KWENYE JAMII YAO

Moja ya jitihada za kuzuia kuenea kwa COVID-19 ilikuwa ni umuhimu wa kila mmoja kuvaa barakoa. Kwa upande wa Zanzibar, inaweza kuwa rahisi kupata barakoa lakini bei zake hazikuwa rafiki kwa walio wengi. Matokeo yake, Wazanzibari wengi hawakuwa na barakoa, na kwa hiyo walijikuta hawawezi kwenda huku na huko kwa uhuru. Jambo hili pia lilipunguza uwezo wao wa kutafuta huduma za afya kwa sababu ya kukosa barakoa, jambo lililowazuia kupata huduma muhimu ya kulinda uhai.




Miza Makame Pandu ni miongoni mwa wanawake 60 mafundi ushoni wenyeji ambao UN Women na Barefoot College waliwapa mafunzo kuhusu stadi za ujasiriamali na elimu ya fedha. ***Picha | Barefoot College***

***Inaendelea Ukurasa wa 10***

*Kutoka ukurasa wa 9*

Ili kushinda changamoto hii, UN Women kwa kushirikiana na Chuo cha Barefoot waliajiri wanawake wenyeji walio mafundi washoni 60 na kuwapatia mafunzo ya ujasiriamali na ujuzi wa fedha. Wanawake hawa walitengeneza na kusambaza zaidi ya barakoa 60,000 (kila mtu alipata mbili) kwa wanajamii 30,000 wa kipato duni, hasa wazee na wanafunzi. Wanawake hawa walilipwa ujira fulani kwa kazi yao hii.

Miza Makame Pandu, fundi mshoni, alijawa na furaha kusambaza barakoa 35 kila siku ili kuisadia jamii yake kujikinga dhidi ya COVID-19. Alisema, “Kwa msaada wa UN Women, nimepata stadi za mambo ya fedha, stadi ambayo sikuwa nayo hapo kabla. Sasa najua kwa nini yanipasa kuweka akiba, na ninajua hatari za kutunza fedha nyumbani.”



Usambazaji wa barakoa katika vijiji mbalimbali vya Zanzibar huku kipaumbele kikiwa kwa wazee na wanafunzi. Vijiji hivyo ni pamoja na Kisiwa Panza, Makoongwe, Kendwa na Matele. ***Picha | Barefoot College***

## UWEZESHAJI VIJANA NA WANAWAKE KIUCHUMI – MAENDELEO YA UJIJI, KIGOMA



Machinjio ya Ujiji yataimarisha uendelezaji mnyororo wa thamani katika Mkoa wa Kigoma. ***Picha | UNCDF/Mariam Simba***

Ujiji ni moja kati ya halmashauri 8 zinazounda Mkoa wa Kigoma na ndiyo halmashauri pekee iliyopanda hadhi na kuwa Manispaa tangu mwaka 2005. Shughuli kuu za kiuchumi katika Mkoa wa Kigoma ni kilimo na ufugaji. Kwa miaka mingi, wakazi wa Ujiji walitegemea machinjio ya zamani ambayo haikuwa na maeneo sahihi ya kuchinjia na kuhifadhia nyama, ukosefu wa maji yanayotiririka, umeme na kukosekana kwa mifumo ya kudhibiti taka. Mazingira haya yaliwaweka wakazi wa halmashauri hiyo katika hatari nyingi.

UNCDF kupitia Programu ya Pamoja (KJP) iliisaidia halmashauri kujenga machinjio mpya ya kisasa ambayo ina uwezo mara mbili wa ile ya awali na ambayo inakidhi viwango vyote vya kiafya na usafi.

Bila shaka mradi huo utafungua fursa kubwa za kiuchumi katika sekta ndogo ya nyama mkoani Kigoma, kutatua hatari za kiafya na kupanua masoko hadi katika nchi jirani.

*Inaendelea Ukurasa wa 11*

*Kutoka ukurasa wa 10*

Fuatilia simulizi ya Bw. Abdillah Mohamedi (32), mfanyabiashara ya nyama kutoka katika Halmashauri ya Manisapaa ya Ujiji akielezea kuhusu hali ya machinjio hasa katika kipindi cha COVID-19. Abdillah hununua kilo 100 kila siku na kwenda kuziuza kwa wafanyabiasahra wadogo, wengi wao wakiwa akina mama. Anasema: "Lilikuwa jambo gumu mno kwetu wafanyabiasahra kwenda kwenye machinjio wakati wa janga (COVID-19) kwani jengo hilo ni dogo jambo lililofanya iwe vigumu kwa watu kuzingatia masharti ya kiafya. Mradi huu ni muhimu kwetu wafanyabiashara kwani litatupa nafasi kubwa zaidi kufanya kazi yetu kwa ufanisi na tija na wakati huohuo kuzingatia masharti ya kiafya."

Mara machinjio mapya yatakapojengwa, Halmashauri ya Manispaa ya Ujiji, itaweza kusimamia sheria ndogondogo zinazokataza uchinjaji katika maeneo yasiyoruhusiwa na kwa hiyo kutengeneza uhitaji mkubwa wa machinjio mpya na kuhakikisha ubora na usalama wa bidhaa.

Kutana na Balibwa Azuhuri Issa (41), mama wa watoto wawili, muuzaji wa rejareja wa nyama na muuza chakula katika machinjio ya Ujiji. Balibwa huuza nyama kwa wanawake wengine wauza chakula wa Ujiji, Kigoma. Balibwa anasema: "Machinjio ya sasa hayakidhi mahitaji kwani haina maeneo ya kutosha kutuwezesha wanawake kufanya biashara zetu kwa ufanisi na kukinga bidhaa zetu dhidi ya mvua. Tunatarajia machinjio mpya yatatatua baadhi ya changamoto zinazowakabili wafanyabiashara hasa akina mama ambao mara nyingine wanalazimika kwenda na watoto wao kwa sababu hawana uwezo wa kuajiri wasaidizi. Anaongeza: "Ujenzi wa machinjio ya kisasa utatoa kipato cha nyongeza kwani idadi ya wafanyabiashara wa nyama na wadau wengine kama wafagiaji itaongezeka. Jambo hili litakuza mtaji wangu na hivyo kunisaidia kukidhi mahitaji ya familia yangu."

Mradi utakuwa na matokeo chanya katika mageuzi ya kiuchumi kwa maana ya ajira, kupunguza umaskini na kuongeza mapato ya serikali ya halmashauri kupitia tozo na kodi mbalimbali.



Balibwa akiwa katika eneo la kuuzia nyama huko Ujiji, Mkoa wa Kigoma. ***Picha | UNCDF/Mariam Simba***

# ILO YATOA MAFUNZO YA UJENZI WA BARABARA KWA WAHANDISI KWA KUTUMIA TEKNOLOJIA YA GHARAMA NAFUU




Dkt. Benelith Mahenge, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, alifanya ziara katika eneo la mradi na kuwahutubia washiriki akiwaasa kutumia vema mafunzo hayo. ***Picha | ILO Tanzania***

Jumla ya Wahandisi wa Ujenzi wa Barabara 20 walishiriki katika mafunzo ya wiki tatu kuhusu Teknolojia ya Ujenzi wa Barabara za Lami za Gharama Nafuu (Low Volume Sealed Roads (LVSR)) huko Chamwino, Dodoma kutoka tarehe 17 Agoisti hadi 5 Septemba, 2020. Mafunzo hayo yaliyoendeshwa kupitia programu ya ILO ya Kuimarisha Uwekezaji katika Ajira (Employment Intensive Investment (EIIP)) iliwaleta washiriki kutoka chuo cha Appropriate Technology Training Institute (ATTI) cha Mbeya, Mamlaka ya Barabara Vijijini na Mijini (Tanzania Rural and Urban Roads Authority (TARURA)), Wizara ya Kazi na Mawasiliano, Mfuko wa Kusaidia Kaya Maskini (Tanzania Social Action Fund (TASAF)), Wizara ya Miundombinu, Ujenzi, Usafirishaji na Mawasiliano, Mfuko wa Uendelezaji Barabara katika TAMISEMI, kampuni za LBT Contractors na PMO-LYED.

Mafunzo yaliendeshwa katika awamu mbili; Awamu ya kwanza ilikuwa zaidi mapitio ya darasani kuhusu masuala ya msingi kuhusu LVSR na awamu ya pili ilikuwa ni kwa vitendo na kwenda ziara kwenye maeneo ya kufundisha kwa vitendo kuhusu LVSR kwa kutumia Mchanganyiko wa Lami Laini (Emulsion Treated Base (ETB)). Jambo hili lilifanyika katika kipande cha mita 100 katika eneo la Chamwino, Mkoani Dodoma.

Kwa mujibu wa Mratibu wa Taifa wa Programu ya EIIP, Bw. Dampu Ndenzako, siyo tu kwamba mafunzo hayo yatahamasiha ajira kamili na zenye tija na kazi zenye hadhi bali pia katika kutatua tatizo linalozidi kukua la ukosefu wa ajira miongoni mwa vijana waume kwa wake nchini.

"...Hili litachangia katika kujifunza njia mbadala zinazowezekana za kiteknolojia

*Inaendelea Ukurasa wa 13*

*Kutoka ukurasa wa 12*

katika ujenzi wa barabara na ukarabati wake na wakati huohuo kuhamisha ujuzi kwa ajili ya uendelezaji wa biashara na uwezekano wa ajira kwa siku za baadaye," alisema.

Katika nyakati za karibuni, ufikikaji hasa katika maeneo ya vijijini umekuwa na changamoto nyingi. Hata hivyo, Tanzania, kupitia Wizara ya Ujenzi na mamlaka nyingine zinazohusika, imewekeza sana katika maendeleo ya miundombinu, ikiwemo upangaji barabara, usanifu, ujenzi, ukarabati na matengenezo ili kuhakikisha kuna ufikikaji bora. Juhudi hizi ni muhimu ili kuhamasisha matumizi ya rasilimali za taifa kwa uimarikaji wa ukuaji wa uchumi.

Akipongeza jitihada hiyo ya utoaji mafunzo kwa vitendo katika eneo la kazi, Katibu Mkuu, Wizara ya Ujenzi, Usafirishaji na Mawasiliano, Mhandisi Elius Mwakalinga, alizipongeza ILO na Serikali ya Ireland kwa kutoa msaada wa kifedha na kiufundi kwa ajili ya juhudi hii mahsusi. "... Teknolojia kama hizi zinavutia matumizi ya njia zinazohamasisha ajira kwa wingi [Labor Based Technology], ambazo zinatengeneza ajira na kipato kwa wanajamii, hasa wale wanyonge, na kwa hiyo kuimarisha viwango vya maisha yao na upatikanaji wa kinga ya kijamii..." alisema.

Programu ya EIIP ya ILO ni moja ya njia za kuhamasisha ajira kamili, zenye tija na zenye hadhi. Programu hiyo ilianzishwa Tanzania mwaka 2016 ili kutatua tatizo la ukosefu wa ajira, kupungua kwa viwango vya mishahara kulikochagizwa na ukuaji uliosababisha udanganyifu wa soko.

Programu hiyo imeendelea kuhamasisha njia za utoaji ajira kwa wingi katika ujenzi wa miundombinu na matengenezo yake kwa sababu 1) ya manufaa yake kijamii (kutengeneza ajira, kinga ya kijamii, kutoa ujira) na 2) njia hii ni bora kiufundi na kifedha katika mazingira a uchumi wa mataifa mengi yanayoendelea leo.



Kama sehemu ya mafunzo, washiriki walishiriki katika ujenzi wa barabara kwa kutumia teknolojia rahisi lakini yenye matokeo mazuri. ***Picha | ILO Tanzania***

# MVUGWE – KUUNGA MKONO UONGOZEZAJI THAMANI YA MAZAO YA KILIMO MIONGONI MWA JAMII ZA PEMBEZONI KATIKA WILAYA YA KASULU



Kituo cha kukusanyia mazao cha Mvugwe kikiwa kwenye hatua ya ujenzi. ***Picha | UNCDF/Mariam Simba***

Kijiji cha Mvugwe ni moja ya vijiji 62 katika Wilaya ya Kasulu chenye jumla ya wakaazi 15,745. Kilimo ndiyo shughuli kuu ya uchumi ambapo kuna wanawake 4,000 na vijana 3,000 wanajishughulisha na kilimo na biashara. Hata hivyo, wakulima wa Kijiji cha Mvugwe wamekwama kwenye lindi la umaskini linalosababishwa na hasara wanayopata baada ya mavuno na uunganishaji duni wa masoko kwa sababu ya kukosekana kwa vituo vya kukusanyia mazao.

Shirika la Umoja wa Mataifa la Mitaji (UNCDF) kupitia Programu ya Pamoja ya Kigoma iliisaidia Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu kujenga kituo cha kisasa cha kukusanyia mazo ili kuwasaidia wakulima wadogowadgo wilayani humo. Kituo cha Kukusanyia Mazao cha Mvugwe kitakuwa kituo kimoja chenye kazi kadhaa kwa ajili ya wauzaji na wanunuaji (wakulima wadogo). Mara baada ya kukamilika, kituo hicho kinatarajiwa kuwa na sehemu za kuhifadhia mazao zenye uwezo wa tani 640, huduma za kukaushia mihogo (vikaushio vya umeme jua), mashine za kusafisha mihogo, maeneo ya kupakia na kupakua mizigo kwenye malori na nafasi kwa ajili ya biashara za rejareja za sekta binafsi.

Kituo cha Mvugwe kitamilikiwa kwa pamoja kati ya Halmashauri ya Wilaya, Serikali ya Kijiji cha Mvugwe na Ushirikia wa Masoko wa Mvugwe. Kupitia umiliki shirikishi (Ushirika wa Umma na Binafsi), kituo kitatoa soko lililo tayari kwa ajili ya wakazi wa kijini (wakulima wadogowadogo) lakini pia kugawanya faida ya kibiashara kwa kuirejesha katika jamii ya Wanamvugwe kwa ujumla.

Kutana na Esta Yosam (36), mkulima kutoka kijiji cha Mvugwe na mnufaika wa Kituo cha Kukusanyia Mazao cha Mvugwe wilayani Kasulu, anasema:

***Inaendelea Ukurasa wa 15***

*Kutoka ukurasa wa 14*

“Kwa sasa tunahifadhi mazao yetu nje ya nyumba, jambo ambalo lina changamoto nyingi hasa wakati wa mvua. Mara nyingine mimi huwa ninapeleka mazao yangu kwenye nyumba ya kaka yangu. Miaka michache iliyopita, wakati wa mavuno nilipoteza magunia 3 ya mahindi. Hiyo ilitokea wakati nilipopeleka mazao yangu sokoni kuuza, na yote hii ilikuwa kwa sababu ya kukosa maghala sahihi ya kuhifadhia.

“Kituo hiki kitawapunguza walanguzi ambao kwa kawaida wanawanyonya wakulima kwa kununua mazao ya wakulima kwa bei ndogo, sasa wakulima na wafanyabiashara wataweza kununua na kuuza mazao moja kwa moja kwenye kituo hicho, jambo litakalowapa bei nzuri yenye utengemao,” Esta anaongeza kwamba: “Wanawake wengi wa vijijini kama mimi, hawakusoma (hawakupata elimu), jambo linalowafanya waendelee kuwa akina mama wa nyumbani na walezi wa familia, naamini kituo hiki kitatoa fursa tofauti na kuwashirikisha katika shughuli za uzalishaji mali kama vile kuuza chakula, kusuka na kuendesha maduka madogomadogo”.

Kituo hicho kitatumika zaidi ya kununua, kuhifadhi na kuuza mazao yasiyochakatwa hadi kuwa yaliyochakatwa, kufungashwa vizuri na kutafuta masoko ya bidhaa zilizochakatwa. Kituo kitatengeneza ajira kwa wanajamii, kuingiza kipato cha ziada kwa wakazi wa Mvugwe na kuongeza chanzo cha mapato ya halmashauri.



Esta Yosam (36), mkulima kutoka Kasulu, na ambaye ni mnufaika wa Kituo cha Kukusanyia Mazao cha Mvugwe, akiwa katika picha. ***Picha | UNCDF/Mariam Simba***

## SIKUKUU ZIJAZO WA KIMATAIFA:

**Desemba 3 –** Siku ya Kimataifa ya Watu Wenye Ulemavu

**Desemba 5 -** Siku ya Kimataifa ya Wanaojitolea

**Desemba 10 -** Siku ya Kimataifa ya Haki za Binadamu

**Desemba 18 -** Siku ya Kimataifa ya Wahamiaji

## UMOJA WA MATAIFA IMARA KWA DUNIA ILIYO BORA ZAIDI

UNITED NATIONS
TANZANIA

**Umoja wa Mataifa Tanzania**

+255 22 219 5021

info.untz@one.un.org

Website: tanzania.un.org

This newsletter is published by the UN Communication Group in Tanzania. To subscribe and provide feedback, please contact us at: info.untz@one.un.org | Website: tanzania.un.org | Tel: (+255) 22-219-5021